

SOMA PIPIYA

OFISI YA RAIS

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA**



Barua zote ziandikwe kwa:
Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya
Simu nambari: +255 (026)- 2702585/2702828
Nukushi, +255(026)-2701776/2700580/270175
Barua pepe: ded@iringadc.go.tz
Tovuti: www.iringadc.go.tz

S.L.P. 108,
IRINGA.
TANZANIA

17/06/2021

**TANGAZO LA KUTAFUTA WASAFIRISHAJI WA MCHANGA NA
KOKOTO**

Kazi Na. LGA/026/ISMANI-H.C/2020-2021/DEV/NC/03

Halmashauri ya Wilaya ya Iringa imepokea fedha kutoka Serikali kuu kiasi cha Shilingi milioni mia nne tu (Tshs. 400,000,000/=) kwa ajili ya Ujenzi wa kituo cha afya ISMANI. Ujenzi utatekelezwa kwa utaratibu wa "Force account". Hivyo, Mganga Mfawidhi wa kituo cha afya Ismani anawatangazia Wasafirishaji wa Mchanga mwembamba na Kokoto kuleta maombi ya kazi hiyo.

MASHARTI YA WAOMBAJI:


1. Mwombaji awe na Mitambo/Gari aina ya Tipper yenye ukubwa wa mita za ujazo nne (4) na kuendelea (Cubic mitre), ambayo itatumika katika usafirishaji wa Mchanga mwembamba na Kokoto.
2. Mwombaji atatakiwa kuwa na wapakiaji wa Mchanga mwembamba na Kokoto katika Gari aina ya Tipper yenye ukubwa wa mita za ujazo nne (4) na kuendelea (Cubic mitre) na atatakiwa kupakia na kusafirisha hadi eneo la Mradi wa ujenzi wa kituo cha afya Ismani lililopo katika Kijiji cha Ismani, Kata ya Kihorogota, Tarafa ya Ismani.
3. Mwombaji atatakiwa kuomba malipo mara baada ya kukamilisha kazi aliyopangiwa ndani ya siku saba (7).
4. Mwombaji anaruhusiwa kuomba kazi mojawapo ya usafirishaji kati ya Mchanga au Kokoto au vyote kwa pamoja.
5. Mwombaji atatakiwa kuonesha bei au gharama ya usafirishaji wa Mchanga mwembamba na Kokoto kutoka eneo la analochukulia hadi eneo la Mradi.

6. Mwombaji atakaye kidhi vigezo atatakiwa kukaguliwa na Mtaalam aliye eneo la mradi kabla ya kushusha Mchanga na Kokoto, endapo hatakaguliwa kazi hiyo haitalipwa.
7. Halmashauri inaweza kufuta maombi ya kazi uliyoomba pale ambapo kutakuwa na sababu za msingi, mfano; bei kuwa juu kupita gharama halisi ya soko, maombi ya kazi uliyoomba kushindwa kukidhi vigezo, kujihusisha na aina yoyote ya udanganyifu au rushwa.
8. **Maombi ya kazi yawasilishwe kwa barua na yaandikwe kwa herufi kubwa** yakionesha aina ya kazi uliyoomba, Jina la fundi au Kikundi na yawekwe kwenye bahasha isiyo na mchoro wala alama yoyote na yafungwe kwa lakili. Aidha bahasha ifungwe vizuri. Pia juu ya bahasha iandikwe jina la kazi uliyoomba. Namba ya kazi husika na anuani ya (KATIBU WA KAMATI YA UNUNUZI, UJENZI WA KITUO CHA AFYA ISMANI, S.L.P 108, IRINGA)
9. Maombi yote yaletwe kwenye Ofisi ya Mganga Mfawidhi wa kituo cha afya Ismani, muda wa kazi kuanzia saa 1.30 asubuhi hadi saa 9.30 Alasiri, Jumatatu hadi Ijumaa.
10. Maombi yote ya kazi yatakayowasilishwa baada ya muda wa mwisho wa kuwasilisha hayatapokelewa.
11. Siku ya mwisho ya kuwasilisha maombi hayo ni tarehe 23/06/2021, saa 5.00 asubuhi na maombi hayo yatafunguliwa hadharani mara tu, baada ya muda wa mwisho wa kuwasilisha.
12. Waombaji wote wanaombwa kuhudhuria katika ufunguzi wa kazi hii katika ukumbi wa kituo cha afya Ismani
13. Gharama ya uchukuaji wa kabrasha la kazi ni Tsh. 20,000/= tu kwa kila ombi, Fedha hii haitarejeshwa.

KURUDISHA ZABUNI

Zabuni zote zirudishwe kwa,

**MGANGA MFAWIDHI WA KITUO,
KITUO CHA AFYA ISMANI,
KATIBU WA KAMATI YA UNUNUZI,
UJENZI WA MAJENGO MANNE (4) YA KITUO CHA AFYA ISMANI,
S.L.P 108.
IRINGA.**


Dr. ACHIA MWENDA